

TANGAZO

Tunapenda kuwajulisha kuwa huduma za Kikonseli kwa waombaji wa hati za kusafiria (Passports) zitatolewa kwa siku 4 kwa wiki (**Jumatatu, Jumanne, Jumatano na Alhamisi**) kuanzia **tarehe 28 Juni, 2021** kwa wale watakaopatiwa miadi. Huduma hizo zitatolewa kuanzia **saa 3:30 asubuhi** hadi **saa 6:30 mchana** na ni kwa ajili ya hatua za kuchukuliwa alama za vidole, picha na kuchukua pasipoti tu.

Hivyo basi, wale ambao wameshawasilisha maombi yao Ubalozini na kupokea uthibitisho kuwa yamepokelewa wanaweza kuomba miadi sasa kupitia barua pepe ppappt@tanzaniaembassy-us.org au kwa simu **2020-884-1080**.

Kabla ya Mwombaji kuanza safari ya kuja Ubalozini ni lazima kupata uthibitisho wa miadi kwa maandishi na kuwa na nyaraka zote zilizoordheshwa katika tovuti yetu www.tanzaniaembassy-us.org

Wale ambao bado hawajawasilisha maombi yao waendeleo na utaratibu wa awali wa kujaza fomu kwenye tovuti ya Uhamiaji www.immigration.go.tz na kutuma fomu hizo na viambatisho vyake vyote kwenye barua pepe ya ubalozi@tanzaniaembassy-us.org.

Aidha, inakumbushwa pia kuzingatia Taratibu za kujikinga na ugonjwa wa Covid 19 kama ilivyoshauriwa na Mamlaka Husika za Nchi Wenyeji.

**UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WASHINGTON, DC**

Juni 25, 2021